## Sasa ni Wakati wa Kubaini na Kukiri Ubaba

Hakuna anayejua kile kinachoweza kutokea katika siku zijazo.

Huwa kuna uwezekano kuwa uhusiano wa wazazi unaweza kuvunjika au kitu kinaweza kutokea kwa mzazi yeyote. Wazazi wanaweza kubaini ubaba katika Tennessee hadi mtoto atakapofikia umri wa miaka 21; hata hivyo, mchakato wa Mpango wa Kukiri Ubaba kwa Hiari (VAoP) upo tu hadi mtoto atakapofikia umri wa miaka 19. Ni kwa manufaa ya mtoto kubaini ubaba mara moja, ikiwezekana wakati wa kuzaliwa.

***IKIWA HUJAOLEWA MTOTO WAKO ANAPOZALIWA, MTOTO WAKO HANA BABA HALALI KIOTOMATIKI.***



## Je, Unahitaji Usaidizi wa Kubaini Ubaba katika Tennessee? Unaweza kupata usaidizi wa Timu ya Usaidizi wa Malezi ya Watoto ya TDHS kwa Kubofya au Kupiga Simu Tu!

**Tembelea Tovuti ya TDHS**

Tovuti ya TDHS ina maelezo ya kuwasaidia wazazi kuanza mchakato wa Kukiri Ubaba kwa Hiari.

Tumia msimbo wa QR kutembelea TN.Gov/HumanServices/For-Families/Child-Support-Services/Tennessee-Paternity-Acknowledgment-Program--TN-Vaop-.html au pata maelezo ya jumla kuhusu mipango ya TDHS katika TN.Gov/HumanServices/families.html.

**Barua pepe:**
ChildSupportPaternity.VAoP.DHS@TN.Gov

**Piga simu kwa:** 833-772-TDHS (8347)

**Mzazi Yoyote wa Tennessee Anaweza Kutuma Ombi la Kupata Huduma za Usaidizi wa Malezi ya Watoto katika:**
OneDHS.Tn.Gov

TN Department of Human Services

**Fuata**
@TNHumanServices

TDHS hutoa fursa sawa na huajiri kwa usawa. Unaweza pia kuandika barua kwa Idara ya Huduma za Binadamu ya Tennessee, Ofisi ya Mshauri Mkuu, Andrew Johnson Tower, 710 James Robertson Pkwy, Nashville, TN 37243, (615) 313-8347.

Idara ya Huduma za Binadamu ya Tennessee, Nambari ya Uidhinishaji. ?, Julai 2019, nakala 0,000. Hati hii ya umma ilipitishwa kwa gharama ya dola 0.00 kwa nakala moja.

TN Department of Human Services

# Kubaini Ubaba

## *Kile Wazazi Wanahitaji Kujua kuhusu Kukiri Ubaba kwa Hiari*



## Ubaba ni Nini?

Ubaba unamaanisha kuwa baba. Ikiwa wazazi wameoana, mume anachukuliwa kuwa baba ya watoto waliozaliwa wakati wa ndoa. Ikiwa baba na mama hawajaoana, hatua za kisheria lazima zichukuliwe ili kubaini ubaba.

## Kubaini (Kukiri) Ubaba ni Muhimu kwa Nini?

### UTAMBULISHO

Watoto wote wana haki ya kujua mama na baba yao na kuwa na uhusiano na wazazi wote wawili. Hisia ya utambulisho na kuwa na mzazi husaidia mtoto kukua kihisia. Uzazi unaweza kuwapa mama na baba hisia ya kuwajibika na kufanikiwa.

### MATIBABU

Kwa kukiri ubaba, mtoto anaweza kujua ikiwa ana magonjwa au matatizo ya kurithi. Mtoto anaweza pia kustahiki bima ya afya ya mama/baba.

### PESA / MANUFAA YA KIFEDHA

Ubaba halali humwezesha mtoto kustahiki kupata manufaa kutoka kwa baba kama vile Usalama wa Kijamii, manufaa ya wanajeshi wastaafu, haki za urithi, bima ya maisha na afya, na usaidizi wa kulea watoto.

## Je, Haki Zako kama Mzazi ni Zipi?

Kusaini fomu ya ubaba ni kwa hiari. Ikiwa wazazi hawajaoana wakati wa kuzaliwa kwa mtoto wao, mama anachukuliwa kuwa mwenye jukumu la ulinzi. Wazazi halali wana haki ya kuwa na uhusiano na kumtembelea mtoto wao. Mara baba anapokiri ubaba, anapata haki hizi. Ikiwa wazazi hawawezi kukubaliana kuhusu jukumu la ulinzi au kutembelea mtoto, wazazi wanaweza kupata Amri ya Mahakama.

## Je, Ubaba Unabainishwaje?

- Wazazi hujaza fomu ya kisheria inayoitwa Kukiri Ubaba kwa Hiari (VAoP) na kusaini fomu hiyo mbele ya mthibitishaji.
- Amri ya Mahakama (ikiwa mzazi yeyote amewasilisha kesi kwa Ofisi ya Usaidizi wa Kulea Watoto ya eneo lako, Ofisi ya Usaidizi wa Kulea Watoto ya eneo lako inaweza kuwasilisha hati zote zinazohitajika ili kupata Amri ya Mahakama, ambayo inaweza kujumuisha kipimo cha DNA.)
- Kipimo cha DNA (Mzazi au Ofisi ya Usaidizi wa Kulea Watoto inaweza kuomba kipimo cha DNA ikiwa uthibitisho wa kibayolojia wa ubaba unahitajika kabla ya mwanamume kutajwa kuwa baba halali.)

Baada ya kupata matokeo ya kipimo cha DNA, ubaba unaweza kubainishwa kwa kutumia VAoP au Amri ya Mahakama.

## Je, Majukumu Yako kama Mzazi ni Yapi?

Wazazi wote wawili wanatakiwa kumlea mtoto wao kutoka wakati wa kuzaliwa kwake. Hii inaweza kujumuisha usaidizi wa kulea watoto, bima ya afya na/au gharama za utunzaji wa watoto. Kila baba na mama anayezaa mtoto anapaswa kukubali sehemu yake ya jukumu la kifedha, kisheria na kihisia.

## Je, Itakuwaje Ikiwa Kuna Mashaka Kuhusu Baba ni Nani?

Ikiwa mzazi yeyote ana shaka yoyote kuhusu baba ni nani, fomu ya VAoP haipaswi kusainiwa. Vipimo vya DNA vinaweza kufanywa ili kubaini ikiwa mwanaume ndiye baba. Ofisi ya Usaidizi wa Kulea Watoto ya eneo lako inaweza kukupa maelezo zaidi, au unaweza kupiga Simu kwa Nambari Maalum ya TN VAoP kwa 1-833-772-TDHS (8347).

## Je, Kukiri Ubaba Kunaweza Kufanywa Wakati Gani na Wapi?

Wakati mzuri wa wazazi kukiri ubaba ni hospitalini mtoto anapozaliwa. Hii inampa mtoto baba halali kutoka wakati anapozaliwa. Jina la baba linawekwa pia kwenye cheti cha kuzaliwa cha mtoto. Wafanyakazi wa hospitali wataelezea mchakato wa kukiri ubaba na kukupa fomu ya kisheria. Unaweza pia kutazama video ya VAoP kabla ya wakati katika: http://tn.gov/ humanservices/article/child-support-establishing- paternity

Ikiwa fomu ya ubaba haikusainiwa hospitalini au una mtoto mkubwa ambaye ungependa kubaini ubaba, mama na baba wanaweza kwenda kwa Idara ya Afya ya eneo lao, Ofisi ya Usaidizi wa Kulea Watoto au Ofisi ya Jimbo ya Rekodi Muhimu ili kusaini fomu.

Kila mzazi lazima asaini fomu mbele ya mthibitishaji, ingawa si lazima wafanye hivyo kwa wakati mmoja. Unaposaini Hati ya Kukiri Ubaba kwa Hiari, lazima utoe hati zifuatazo:

1. Kitambulisho cha picha, kama vile leseni ya udereva.

2. Nambari yako ya Usalama wa Kijamii.

## Je, Itakuwaje Wazazi Wakikiri Ubaba Lakini Baadaye Wakabadili Mawazo Yao?

Wazazi wanapaswa kufikiria kwa makini kabla ya kukiri ubaba. Ikiwa mzazi yeyote atabadilisha mawazo yake, ana siku 60 za kubatilisha (kughairi) uthibitisho huo kwa maandishi.

Tumia msimbo wa QR ulio hapa chini ili upate maelezo zaidi kuhusu Kukiri Ubaba kwa Hiari kwa Wazazi wa Tennessee.